# Ufungwa wa Kisaikolojia katika Riwaya ya Takadini

**Zuhura Said**
Chuo Kikuu cha Dodoma
*saidzuhurat@gmail.com*

***Ikisiri***
*Makala haya yamechunguza suala la ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya ya Takadini. Tatizo hasa ni kwamba dhana ya ufungwa ilichunguzwa zaidi na wataalamu waaliotangulia katika mwegamo wa jela. Suala la ufungwa wa kisaikolojia halikushughulikiwa kwa mapana yake. Hata hivyo, makala yamejiegemeza katika mkabala wa kitaamuli. Data zimepatikana kwa njia ya uchambuzi wa matini. Nadharia ya Saikolojia Changanuzi imetumika katika uchambuzi wa data zilizowasilishwa. Matokeo ya uchunguzi huu yameonesha kuwa ufungwa wa kisaikolojia umegawanyika katika makundi makuu mawili. Makundi hayo ni ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala na ufungwa wa kisaikolojia usio wa kijaala. Ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala ndio ambao umemakinikiwa zaidi katika makala haya. Aina ya pili imedokezwa tu ili kujenga msingi wa hoja. Aidha, matokeo ya uchunguzi yanadhihirisha kuwa kila mwanadamu ni mfungwa kwa kuwa hakuna mwenye uhuru uliokamilika. Hali hii inatokana na kukabiliwa na mamlaka, kanuni, sheria au taratibu zinazompangia mwanadamu asifanye baadhi ya mambo, ambayo anahisi anawiwa kuyafanya. Makala yanahitimisha kuwa kila mtu huangukia katika ufungwa wa aina mbalimbali kwa sababu ya kushindwa kutimiza matamanio ya nafsi yake kwa namna aitakayo. Matokeo yake hujikuta akiangukia katika manung'uniko, mafumbo na kusema bila kuzingatia taratibu, utamaduni na staha za jamii inayohusika.*

**Maneno Muhimu:** Ufungwa wa kisaikolojia, nadharia ya ufungwa, mkondo wa ufungwa na riwaya ya ufungwa.

## 1.0 Utangulizi

Ufungwa ni kipengele kimojawapo kinaweza kuhakikiwa katika kazi za kifasihi. Dhana hii inaweza kuhakikiwa kwa kigezo cha kifani au cha kimaudhui (Said & Taib, 2019). Dhana ya ufungwa katika fasihi ilianza kuchunguzwa kama dhana inayojihusisha na maudhui ya kijela katika kazi za kifasihi. Pia, Madumulla (2009) anaihusisha dhana hiyo kama sehemu ya mapito ya riwaya ya Kiswahili. Katika kuihakiki dhana hiyo, wataalamu wengi walijikita kuihakiki kama dhana inayotokana na kazi mbalimbali za kifasihi zinazohusu masuala ya jela tu (Mulokozi, 2017). Makala haya yatatoa ufafanuzi kuwa dhana ya ufungwa haijinasibishi tu na jela pia inahusisha hali ya kutokuwa huru kwa saikolojia binafsi ya mtu. Hii ina maana kwamba dhana ya ufungwa ni pana mno kwa sababu inarejelewa na suala la kukosekana kwa uhuru. Hivyo, saikolojia ya mtu pia inaweza kukosa uhuru katika kufanya maamuzi juu ya jambo fulani, kutenda na hata kunena. Inapotokea mtu anatamani kufanya jambo fulani kulingana na matakwa yake, ama matakwa hayo yawe mazuri au mabaya lakini anashindwa kujitimizia kwa uhuru autakao, hali hiyo ndiyo iitwayo ufungwa wa kisaikolojia. Huu ni ufungwa wa kisaikolojia kwa sababu hamu na matamanio yapo ndani ya nafsi yake. Hii ni kusema kuwa kuchukia au kutamani kupo ndani ya nafsi ya mtu husika na hivyo hayadhihiriki kwa uwazi isipokuwa kwa viashiria. Shabaha kuu ni kubainisha aina mojawapo ya ufungwa wa kisaikolojia kati ya mbili zilizojitokeza katika riwaya ya *Takadini*. Ni kwa msingi huo, maudhui ya makala haya yatapanua uelewa kwa wanataaluma na wanafunzi katika kuielewa dhana ya ufungwa wanapohakiki kazi mbalimbali za kifasihi. Zaidi pia, maudhui yatapunguza udumavu wa kifikra uliojengeka miongoni mwa wanataaluma, kuwa dhana hii ni dhana inayohakikiwa kwa mtazamo wa jela

tu. Hoja kuu ya makala hii ni kuwa ufungwa wa kisaikolojia unadhihirika katika riwaya ya Kiswahili. Ufungwa huu ndio ufungwa wenye mawanda mapana zaidi. Kutokana na hili, imegundulika kila maisha ya mwanadamu yameandamwa na ufungwa wa kisaikolojia. Hii ina maana ya kwamba matamanio ya kila mtu yamedhibitiwa na nguvu za asili za kimamlaka au za kutengenezwa zinazo mtawala mtu huyo. Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni: utangulizi, uwasilishaji wa data (ufungwa wa kisaikolojia), na hitimisho.

## 1.1 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umetumia Nadharia ya Saikolojia Changanuzi. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), nadharia hii iliwekewa msingi na mwanasaikolojia wa Austria, Sigmund Freud (1856–1939). Misingi ya Nadharia hii iliendelezwa na Karl Jung (1875–1961) na Jacques Lacan (1901–1981). Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ilianza kutumika miaka ya 1896 na kuendelea kutumika katika karne ya ishirini ya 20 (Wamitila, 2002). Hii ni nadharia inayotumia dhana na mitazamo ya kisaikolojia kuchambua kazi za fasihi. Freud anadai kuwa akili ya mwanadamu imegawika katika nafsi tatu, ambazo ni: nafsi ya matamanio, nafsi ya urazini na nafsi ya kimaadili (Mulokozi, 2017).

Nafsi ya matamanio ni nafsi yenye kubeba matamanio yote ya mtu bila kujali urazini wala itikeli za kijamii. Katika nafsi hii ndimo fikra nyingi na mawazo mengi hasi hubuniwa na kuhifadhiwa. Mawazo hayo hujitokeza kiishara katika ndoto, utani, sanaa, au uandishi na mitelezo ya kauli (Buliba, 2014; Mulokozi, 2017; Wamitila, 2002). Hivyo, Freud anafananisha usanii na njozi zinazoashiria matumaini na matamanio ya mtu, ambayo yametoka katika nafsi hiyo ya matamanio. Nafsi ya mtu inapokosa uhuru binafsi wa kujiamulia mambo kutokana

na mikatale iliyowekwa na jamii, ili kutosheleza mataratajio na kuukamilisha uhuru uliokosekana, matamanio hayo huwasilishwa kwa njia ya kuandika (Wafula na Njogu, 2007).

Nafsi ya pili ni nafsi ya urazini, hii ni nafsi ya utashi, busara na tafakuri. Ndiyo nafsi imfanyayo mwanadamu asitende mambo mbalimbali ambayo hayakubaliki kwa jamii (Wafula na Njogu, 2007; Wamitila, 2002). Nafsi nyingine ni nafsi ya kimaadili. Hii huchunguza uadilifu wa tendo linalotarajiwa kufanywa, wema na ubaya wake, kabla halijatendeka. Nafsi hii inaweka mipaka ya ustaarabu wa jamii, hivyo, husimamia mbeko za kimaadili katika jamii (Buliba, 2014; Mulokozi, 2017; Wamitila, 2002). Kwa jumla, nafsi hizi tatu ndizo msingi na mhimiri mkuu ulioongoza kuchambua, kuwasilisha data na mjadala wa matokeo ya utafiti huu. Kupitia nafsi hizi tatu kama kigezo cha msingi cha nadharia hii, mtafiti aliweza kubainisha aina za ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya ya *Takadini*.

## 2.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti uliozaa makala haya ni wa kifenomenolojia. Usanifu huu hujishughulisha na uchambuzi na ukusanyaji wa data kwa kuhusishwa na uzoefu, ambao binadamu wanao katika kuhoji na kuhukumu masuala au mitazamo mbalimbali iwazungukayo katika maisha yao ya kila siku. Usanifu wa kifinomenolojia hujikita zaidi katika ufafanuzi wa tafiti zilizo katika mawanda ya kijamii kama vile Insia, Sosholojia na Saikolojia (Ponera, 2019). Usanifu huu umetumika kwa sababu shabaha yake, asili ya mada na malengo yake vimejielekeza katika mwegamo wa kisaikolojia. Makala haya yameongozwa na mkabala wa kitaamuli, yaani maelezo yametumika zaidi kuliko taarifa za kitakwimu katika kujenga maudhui yake (Ponera, 2019). Data za utafiti zimekusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti

kuchambua riwaya ya *Takadini* (2003) iliyoandikwa na Ben Hanson na kubainisha aina za ufungwa wa kisaikolojia unaojitokeza katika riwaya hiyo, ambalo ndio lengo mahsusi la makala haya. Riwaya hii imeteuliwa kwa sababu ya utoshelevu wake wa mdhihiriko wa aina za ufungwa wa kisaikolojia katika riwaya hiyo.

## 3.0 Ufungwa wa Kisaikolojia katika Riwaya Teule

Katika kipengele hiki, ufungwa wa kisaikolojia uliojitokeza katika riwaya ya *Takadini* umejadiliwa. Kwa jumla, ufungwa wa kisaikolojia umegawanyika katika aina kuu mbili: aina ya kwanza ni ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala na aina ya pili ni ufungwa wa kisaikolojia usio wa kijaala. Ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala umetokana na neno jaala lenye maana ya kuwepo kwa nguvu maalumu, ambayo inatokana na Mwenyezi Mungu. Kuwepo kwa kani hiyo hakutegemei nguvu wala mamlaka ya mtu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004) inafafanua neno jaala kama mambo ayafanyao mtu kwa kutegemea uwezo wa Mungu. Ujaala ni dhana inayojinasibisha na itikadi ya kidini ya mwanadamu, ambapo huamini kuwa vitu na mambo yote yaliyoko na ayatendayo katika dunia yake, ni majaaliwa: ni kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu (Duwe, 2020). Katika kufafanua dhana hii, Wamitila (2002) anasema wana ujaala wanaamini kuwa maisha ya mwanadamu pamoja na matendo yote ayatendayo katika ulimwengu wake, vinatawaliwa na kuongozwa na nguvu za Mwenyezi Mungu. Kwa upande mwingine, Duwe (2020) anadai kuwa mwanadamu hawezi kufanya jambo lolote katika maisha yake bila kutegemea nguvu za kijaala. Duwe anaendelea kusema kuwa fikra za kijaala zinajipenyeza katika fikra za mwanadamu ambapo anayatazama maisha kuanzia mwanzo hadi hatima (mwisho) yake kwa kujiegemeza katika imani ya nguvu na uwezo wa Mungu wake. Kwa hiyo, aina hiyo

imeiitwa hivi kwa sababu nguvu ya kufunga anayo yeye (Muumba wa mbingu na ardhi) na mtu mwingine anapaswa kutii hata kama hataki kufanya hivyo. Mathalani suala la kuzaa na kuzaliwa, mchakato wa kukua kwa mtoto, kuumwa, kufa na kuzikwa hakuna anayepanga awe au asiwe na mambo hayo isipokuwa inatokea tu. Kwa kuhitimisha hili, Sengo (h.t) katika kitabu chake kiitwacho *Mke ni Waziri Mkuu Nyumbani* mwake anasema kuwa:

> *Aliyeumba na kupanga yote ya Ulimwengu wake, hajamruhusu insi wala jini kutenguwa usiku kuwa mchana, mchana kuwa usiku; mbingu kuwa ardhi, ardhi kuwa mbingu, mwanaume kuwa mwanamke, mwanamke kuwa mwanaume, mtoto kuwa mzazi wa mzazi wake wala mzazi kuzaliwa na mwanawe. Aliyeumba kayaumba yeye na alitakalo yeye vyovyote, kokote, ndilo liwalo. Kasema Laa haula wala quwata ilaa billah. Alitakalo ndilo liwalo.*

Maelezo haya ya Sengo yanadhihirisha waziwazi kuwa ufungwa wa kijaala wa kisaikolojia unatokana na Mwenyezi Mungu, mwenye mamlaka ya kila kitu.

Aidha, ufungwa usio wa kijaala wa Kisaikolojia ni kinyume na aina ile ya kwanza ya ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala. Ufungwa huu hausababishwi na Mwenyezi Mungu bali unasababishwa na kanuni na sheria mbalimbali zilizotungwa na mwanadamu mwenyewe. Hivyo basi, mwanadamu hujikuta akifungwa kwa kujua au kwa kutokujua, hii inatokana na mipaka au vizuizi mbalimbali vinavyotokana na kanuni na sheria hizo. Kanuni au sheria hizo zinazomuwekea mipaka huenda zikawa zimewekwa na yeye mwenyewe au jamii yake. Kutokana na mipaka na vizuizi hivyo, mwanadamu hujikuta akifanya mambo mbalimbali si kwa matakwa yake bali kwa sababu jamii inayomzunguka humtaka afanye hivyo na asifanye

vile. Kwa hiyo, katika makala haya aina ya kwanza (ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala) ndio ulio makinikiwa katika makala haya. Kwa maaana hiyo, aina ya pili ya ufungwa wa kisaikolojia (usio wa kijaala) imedokezwa tu ili ijulikane kuwa inapojadiliwa kuhusu aina kuu za ufungwa wa kisaikolojia basi ufungwa usio wa kijaala ni aina pacha ya ufungwa huo. Hivyo basi, katika aya zifuatazo ufungwa wa kisaikilojia wa kijaala na namna umejadiliwa kwa namna unavyojitokeza katika riwaya ya *Takadini*.

## 3.1 Ufungwa wa Kisaikolojia wa Kijaala

Kama ilivyofafanuliwa katika aya zilizotangulia, ufungwa huu hutokana na nguvu na mamlaka ya ki-uungu. Ufungwa huu nao umegawanyika katika aina kuu tatu: wa kibaiolojia, wa kijiografia na wa kiitikadi. Aina hizi zote zimejitokeza katika riwaya ya *Takadini* kama ambavyo imefafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.1.1 Ufungwa wa kisaikolojia wa kibaiolojia

Ufungwa huu ni ufungwa unaotokana na asili. Ni ufungwa wa kibaiolojia kwa sababu utokeaji wake huwa ni wa asili. Kinachomfunga mtu hakiwezi kufunguka kwa namna yoyote ile. Miongoni mwa mambo yanayounda ufungwa huu ni pamoja na kuzaliwa, kuumwa, kufariki na michakato yote ya kibaiolojia. Kwa mfano, hakuna mtu ambaye ana uhuru wa kujiumba wa jinsi au wa tambo fulani, mathalani kuwa mwanamke au mwanaume, mfupi au mrefu, mnene au mwembamba, mweusi au mweupe. Ufungwa huu unajitokeza katika riwaya teule kama inavyoonekana katika aya inayofuata.

Katika riwaya ya *Takadini* suala la ufungwa wa kibaiolojia limejitokeza katika tukio la Mzee Makwati alipotafuta mtoto wa kiume kwa miaka mingi na wake zake wengine watatu walishindwa kumpatia kwa kipindi chote ambacho wameishi.

Vilevile, ufungwa wa kibaiolojia umejitokeza kwa wake wa Makwati ambao ni: Rumbidzai, Dadirai, na Pindai kwa kushindwa kumpatia mtoto wa kiume mume wao ijapokuwa kila mmoja alitamani awe wa kwanza kumpatia Makwati mtoto wa kiume. Vilevile, ufungwa huu ulikuwa kwa Makwati kukaa muda wa miaka tisa katika hali ya utasa jambo, ambalo liliwafanya wake wenzake wamsimange. Katika ukurasa wa nne (4), mwandishi anasema, "siku zote alikuwa mwenye furaha, ingawa kukosa mtoto kulipingana na fikra zake njema."

Katika maisha halisi tunaona namna watu mbalimbali wanavyohangaika kuwatafuta watoto. Pia, wengine wanatafuta aina fulani ya watoto; kike au kiume. Matokeo ya kukosa watoto wengi wao hujikuta wakienda kwa waganga na kuomba miungu ya aina mbalimbali ili mradi kukidhi matamanio ya kuwa na mtoto (kwa asiye naye) au ili apate aina fulani ya mtoto. Kitendo cha watu kuhangaika hivi ni matokeo ya kuukosa uhuru wa kuamua kuwa na aina fulani ya mtoto amtakaye. Laiti kama wangekuwa huru bila shaka kila mmoja angeridhika na alichonacho.

Vilevile, katika nukuu inayofuata mwandishi anaonesha ufungwa alionao Sekai juu ya kiumbe kilichomo katika tumbo lake hajui kuwa ni kiumbe gani ijapokuwa anapenda kujua. Mwandishi anasema:

> *Ndiyo Pindai, ninaogopa…Nani anayeweza kujua kilichomo tumboni mwa mwanamke? Hivi sasa ndio nahisi ajabu kubeba mtoto mchanga katika mwili wangu. Lakini hilo haliachi kutisha maana hujui kiumbe hicho kitakuwaje. Je atakuwa wa kike? Au wa kiume? Atakuwa wa kawaida au mwenye kasoro? Lakini kibaya zaidi, kiumbe hicho kitakuwa binadamu?Nimeshawahi kusikia kuhusu wanawake wanaojifungua viumbe wa ajabu* (Uk. 3).

Katika nukuu hii inatuonesha namna suala la kubeba ujauzito na kujifungua ni suala lililofungwa. Sekai amefungwa hakujua ndani ya tumbo lake kutakuwa na nini. Kwa upande mwingine, Sekai na mumewe Makwati walitamani mtoto wa kiume kwa miaka mingi lakini hawakupata muda ambao wao waliutaka. Na muda ulipofika, hakikuzaliwa kiumbe walichokitaka badala yake walizaa mtoto *sope (*Uk. wa 1 hadi 9). Kwa sababu hiyo, Sekai mwenyewe, mumewe (Makwati) na jamii kwa ujumla walitamani Sekai azae mtoto wa kawaida na sio *sope*, lakini majaliwa ya Mungu yamewafunga wote kwa kuwa hawakupenda kuzaa *sope*.

Ufungwa huu pia unajitokeza katika ukurasa wa 27 kwa Chivero na Shuvai walitamani mtoto wa kiume badala yake walipata mapacha. Jambo hili kwao lilikuwa ni laana. Hivyo, walilazimika kumuua mtoto mmoja; wa kike na kumbakiza wa kiume, aliyekuwa anatakiwa. Aidha, suala la kuzaa mtoto wa jinsi fulani si suala la matakwa ya mtu bali inatokea kulingana na majaaliwa ya Mwenyezi Mungu. Quran tukufu katika sura ya thelathini na moja (Luquman) aya ya thelathini na nne inasema, “Hakika Allah pekee ndiye anajua kiumbe gani kipo ndani ya mfuko wa uzazi wa mama.” Katika nukuu hiyo, binadamu ananyimwa uhuru wa kujua chochote kuhusu kiumbe kilichomo tumboni. Haya hiyo inasisitiza kuwa mamlaka ya kujua aina ya kiumbe kilichomo ndani ya tumbo la mama mjamzito ni la Mwenyezi Mungu pekee; hivyo, Yeye ndiye anayejua rangi, umbile, au jinsi ya kiumbe hicho.

Hapa ni kwamba suala la uhuru wa mwanadamu ni suala muhimu sana ijapokuwa uhuru wa asilimia zote haupo. Inapotokea mtu anashindwa kufikia kiwango fulani cha uhuru anaoutafuta hujikuta akiingia kwenye msongo wa mawazo.

Mauki (2020) akimnukuu Herman (2012) anafafanua kuwa msongo wa mawazo ni "hali ya hatari anayohisi mtu mbele yake, ambayo inaambatana na hali ya woga, kukosa furaha, amani, mtikisiko wa kihisia pamoja na kujisikia ugumu katika kurudia hali ya kawaida." Msongo wa mawazo ukiwa wa kawaida humfanya mwanadamu aendelee kuwaza namna ya kujinasua hapa ndipo uvumbuzi wa mambo mbalimbali ya kitekinolojia hutokea. Kwa mfano, uvumbuzi wa mashine kama *Utrasound* ni ishara kuwa mwadamu ni mfungwa. Hivyo basi, katika kuutafuta uhuru wake unaotokana na mambo ya kijaala kama hayo ya uzazi, mwanadamu hukimbilia kwenye zana za kiteknolojia ili kujinasua na ufungwa alionao. Kufanya hivyo kunampa auheni ya kifungo chake kwa sababu angalau atajuzwa kuhusu aina ya mtoto aliyepo tumboni kupitia kipimo hicho ijapokuwa si kwa asilimia zote ila kwa kubahatisha tu.

Vilevile, suala la kuwa na kutokuwa na mtoto ni suala la kijaala, kama ambavyo riwaya *Takadini* imechora hali hiyo. Ufungwa huu umekuwa ukisababisha watu kuachika katika ndoa kila siku, lakini kwa sababu tu hawana uhuru wa kutimiza matakwa yao, hujikuta wakifanya maamuzi yasiyo sahihi kama vile kufanya shirki, kujiua, na kadhalika. Katika kuthibitisha hoja hii Quran inasema:

> *Ni mfalme wa Allah wa mbinguni na ardhini, anaumba kadri anavyotaka mwenyewe, anampa amtakaye watoto wa kike watupu, na anampa mwingine watoto wa kiume watupu au anamchanganyia wa kike na wa kiume na anamjaalia mwingine kuwa tasa (asiyezaa, hakika yeye Allah ni mjuzi na mwenye kukadiria* (Quran, 49–50).

Katika nukuu hii inatudhihirishia kuwa suala la kuzaa na mchakato wake ni suala linalopangwa na Mwenyezi Mungu; binadamu hawezi kujinasua katika kifungo hicho ata kama angetaka kufanya hivyo. Kwa mfano, suala la kuzaa kwa uchungu, Hanson anasema:

> *Kabla ya hapo, Sekai hakuwahi kupatwa na maumivu kama hayo. Kadiri muda ulivyopita, ndivyo maumivu yalivyozidi kuongezeka. Awali, aliwahi kuchomwa na mwiba uliomsababishia kidonda chenye maumivu makali kwa siku tatu. Katika tukio jingine, jino lake lililovunjika lilimuuma. Maumivu hayo yalikuwa makubwa kuliko yale ya mguuni. Lakini kwa uchungu wa uzazi -mai - we - e! Ni uchungu kuliko maumivu yote hayo. Ingawa maumivu hayo ni makali na yakutisha lakini ni yenye furaha kubwa* (Uk. 7).

Ufungwa huu pia unahalisika katika jamii zetu. Suala la mwanamke kuzaa kwa uchungu ni suala la kiufungwa kwa sababu hakuna mwanamke apendaye maumivu ya uchungu ya uzazi ila kwa kuwa hakuna namna ya kujizuia wanawake hulazimika kuzaa kwa uchungu. Hata hivyo, katika kujinasua katika ufungwa huo, wapo baadhi ya wanawake wanaokwepa jambo hilo na hatimaye kuwafuata madaktari wawazalishe kabla ya muda kwa njia ya upasuaji ili kukwepa maumivu hayo.

### 3.1.2 Ufungwa wa kisaikolojia wa kiitikadi/kitamaduni

Hii ni aina nyingine ya ufungwa wa kisaikolojia wa kijaala. Aina hii inatokana na mikatale ya dini au tamaduni. Ni ufungwa wa kijaala kwa sababu sheria au kanuni zinazomfunga mtu zinatokana na nguvu fulani ya kiuungu, kimizimu na kiuhenga. Ufungwa huu umejitokeza katika riwaya hii. Mila na desturi za mtemi Makwati zinahalalisha mwanamke asiyezaa miaka tisa auawe. Kwao, mwanamke wa namna hiyo ni nuksi katika jamii.

Kutokana na sheria hii, mwandishi anawachora wake wenzie na Sekai katika harakati za utekelezaji wa sheria hiyo. Wanawake hawa walitamani Sekai auawe kwa sababu ya kutozaa kwa miaka tisa. Watu hawa wamefungwa na mila na desturi kwa sababu sheria za kimila zinawalazimisha kutii hata kama hawataki kutii. Mwandishi anasema:

> *Watu wengine wapo tayari kufanya chochote ili mradi kubaki na mume. Nina uhakika kuwa ng'ombe yoyote aliyeshindwa kuzaa kwa miaka tisa, angekwisha uawa na kuliwa zamani. ...ni mwanamke mchawi tu ndiye anayeweza kubaki na mume kwa muda mrefu hivyo bila kuzaa* (Uk 2).

Nukuu hiyo inaonesha wake wenzie Sekai wamefungwa na mila na desturi zao. Hii imetokana na kuamini kuwa mwanamke yeyote anayechelewa kuzaa kwa miaka tisa lazima auawe kwa sababu mila na desturi zao zinataka hivyo.

Vilevile, ufungwa huu unajitokeza pindi Sekai amezaa *sope*. Sekai alitakiwa atengwe na mtoto wake kwa sababu ni *sope*. Hii ni kwa kuwa mizimu yao inaamrisha hivyo, na jambo hili lilikuwa la jamii nzima kuanzia Makwati mwenyewe, wake wenzie Sekai, wakunga na jamii kwa ujumla. Mwandishi anasema hivi:

> *Ninachokumbuka, wakati nikichezwa unyago, mwalimu wetu kiongozi aliwahi kutufundisha juu ya mtoto wa aina hii. Aliyezaliwa bila ngozi aliondolewa na kutengwa mbali na mama yake* (Uk. 8).

Vilevile, Sekai alitakiwa kuuawa yeye pamoja na mtoto kwa kuwa ni *sope* wakidai kuwa mizimu ndivyo ilivyoamrisha. "Lakini Sekai endapo wataamua mtoto hata wewe utauawa kwa sababu ya kupinga sheria za kale"

(Uk.18). Pia, ufungwa huu unajidhihirisha katika ukurasa wa 28 wakati Chivero akithibitisha kuwa watoto masope hawakuhitajika hata katika jamii yao tangu enzi anasema, *"Sijawahi kumuona yeyote kama huyu, na kwa nini? Kwa sababu watu wetu huwaharibu upesi mara tu baada ya kuzaliwa.Wako tofauti na hawafai katika jamii."*

Ufungwa wa kiitikadi unajitokeza pale ambapo mkunga Ambuya na Makwati wanaamini kuwa kuna siku maalumu kwa mwanamke aliyejifungua kumuona mumewe. Pia, kuna siku maalumu ya kumuona mtoto kwa mwanaume ambaye mkewe ametoka kujifungua. Kwa mantiki hii hata kama mume au mke wametamani kuonana hawana budi kutekeleza masharti ya mila na desturi zao. Haya yanajidhihirisha katika nukuu hii:

> *"Hivi sasa nakuomba unipatie maji nioge ili nimfuate mume wangu atakaporejea lakini huwezi kufanya hivyo. Muda wa kuonana naye haujafika bado. Haruhusiwi kumwona mtoto mapema kiasi hiki," Ambuya Tukai alimsihi… Lakini mbona umekuja kuniona mapema hivi? au mtoto wetu anaumwa? Aliuliza huku hofu ikidhihirika katika sauti yake* (Uk 10).

Vilevile, ufungwa huu unajitokeza pale Makwati anapoamini kuwa mwanamke anayezaa *sope* lazima awe amechepuka na mwanaume mwingine au kwa kuwa aliishi na mwanamke tasa hivyo ni laana ya mizimu. Makwati amefungwa kitamaduni kiasi cha kuamini kuwa mkewe alimsaliti na kuchepuka na mwanaume mwingine ndio maana amezaa mlemavu wa ngozi, jambo ambalo halina ukweli wowote isipokuwa mila na desturi tu ndio zinamfanya amini hivyo. Mwandishi anasema:

> *Bila ngozi, sope? Hilo sitalielewa. Inawezekanaje? Sema we mwanamke! Ni kipi ulichokileta kwetu? Kama unasema ukweli yuko wapi mtoto huyo? Ama uchawi au laana ya mizimu? Kwa nini huyo sope yungali nasi? ... Makwati alijizuia kumsogelea na kumgusa mwanamke aliyempenda kuliko wote…Iweje awe kama mimi kisha tena tofauti? Labda mke wangu amelogwa au hii ni laana ya mizimu yetu kwa kuwa nimeishi na mwanamke tasa…* (Uk. 11–13 na uk. wa 41).

Wakati huohuo wake zake Makwati wanaamini pia kuzaa *sope* ni kwa sababu Sekai alikunywa maziwa mengi pindi akiwa mjamzito au kwa kuwa alikataa mwanaume wa kuchaguliwa na wazazi wake hivyo mizimu imemlaani. Nukuu ifuatayo inajidhihirisha:

> *Kama ni mimi, ningemrejesha kwa mizimu mara moja… yawezekana hana tatizo lolote lile, labda alikunywa maziwa mengi wakati wa ujauzito… Hakutaka kuolewa na mtu aliye chaguliwa na wazazi wake. Alidhani yeye ni mzuri sana, mzuri mno kwake. Lazima atimuliwe hapa arudi kwao, atimuliwe tena?Ni mchawi, wote yeye na dubwasha lake lazima wauwawe. Hafai kuachiwa amnase mwanaume mwingine. Kwa njia yoyote ile lazima atokomezwe milele katika siku chache zijazo* (Uk. 15).

Pia, ufungwa wa kitamaduni unajitokeza pale kwa Chivero na Shuvai walipozaa mapacha, lakini mtoto mmoja wa kiume alitupwa na jamii yao wakiamini ni laana kuzaa mapacha. Kwa hiyo, wahusika hawa nafsi zao hazikupenda mtoto wao atupwe ila walishindwa kuzuia kwa sababu maamuzi ya jambo hilo lilikuwa chini ya tamaduni zao. Mwandishi anasema:

> *"Walikuwa wawili," mkewe alimweleza, tulipata wa kiume pia, lakini Ambuya alimtupa" kwani walimpeleka wapi? Aliuliza wakati ule angali katika umbumbu wa ujana..." "...Sote tunajua mila za mababu zetu katika kila koo na kijiji. Watoto kama huyu lazima wauwawe, wenye ulemavu lazima wauawe, hata pacha mmoja lazima auawe," ...Kama haturuhusu mbegu yoyote ya aina hiyo kuishi miongoni mwetu, tutawezaje kuruhusu mgeni aishi kati yetu…"* (Uk. 27 na 33).

Fauka ya hayo, mwandishi anaonesha ufungwa wa kimila katika ukurasa wa 32. Hapa Chivero anawaasa wanajamii kuhusu kuwepo kwa sheria za mababu zao kuhusu kumfukuza mgeni, ambaye anahitaji msaada. Pia, katika ukurasa wa 47, mhusika Tendai analazimishwa kuolewa na mwanaume ambaye ni sawa na baba yake mzazi. Kutokana na hilo hafurahishwi na masuala ya ndoa kutokana na umri wake mdogo ila amefanya hivyo kwa sababu tu ya heshima ya kuwa mke wa mtemi. Mwandishi anasema:

> *"Je, unampenda mtemi Masasa?... Tendai alisita kwanza kujibu. "Ni heshima kuwa mke wa mtemi mwenye nguvu kama Masasa. Lakini namchukulia kama baba yangu kuliko mume wangu." Je, unayo furaha kuwa hapa? Tendai alipasua jipu, "Wake wenzangu ni kama mama zangu. Siku zote wananitazama mimi, wananikaripia, na mabinti zao ambao ni wa umri wangu hucheka kwa dharau kila wanitazamapo. Wasichana wengine hunikimbia kwa kuwa mimi ni mke wa mtemi..."* (Uk. 32).

Katika nukuu hiyo ni wazi kuwa Tendai hafurahii maisha ya ndoa ila amekubaliana na hali hiyo kwa sababu ya tamaduni zao. Aidha, suala la kuwa mke wa mtemi linamfanya asiwe

huru kucheza na watoto wenzake na kupewa heshima kubwa, ambayo hailingani na umri wake.

### 3.1.3 Ufungwa wa kisaikolojia wa kijiografia

Ufungwa wa kisaikolojia wa kijiografia ni ufungwa unaotokana na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na maumbile ya kijiografia na namna yanavyochukuliwa na mwanadamu. Kwa mfano, hali ya kuwepo kwa kiangazi au masika, usiku na mchana, mvua au jua, mwezi au giza, baridi au joto, kupatwa kwa jua, kujaa na kupwa kwa maji, na kadhalika. Pia, kuwepo kwa milima, tambarale, misitu, bahari, maziwa, mito na majangwa. Hali zote zimekuwa zikiminya uhuru binafsi wa mtu kwa namna mbalimbali.

Hali hii inadhihirika katika maisha halisi ya watu namna ambavyo wakilaani mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa mfano, kuna misemo kama: *mji huu una joto sana, mji huu una baridi, jamani mvua hii haiishi, leo kuna joto kali sana au leo kuna baridi sana.* Hali hizi zote zimekuwa zikitokea tu hakuna apangaye. Kwa kuwa hakuna apangaye bali ni majaaliwa ndio maana kila mmoja huwa na namna yake ya kufungwa kulingana na maono yake kuhusu hali fulani. Ufungwa huu unajitokeza ukurasa wa 55, ambapo Takadini hakupenda hali ya hewa ya joto na kuwepo kwa jua kwa sababu mwanga wake ulikuwa unatesa macho yake. Mwandishi anasema:

> *Takadini alitaabika sana wakati wa mwanga wa jua la kiangazi. Macho yake yalifumba kukwepa mwanga huo mkali. Pia aliumizwa na joto la jua kiasi ambacho shingo yake ilienea michubuko sawa na mikono, mbavu, magoti na viungo vya mikono* (Uk. 55).

Nukuu hiyo inadhihirisha ufungwa wa kijiografia unaotokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Wakati hali ya joto na jua kali ikimsumbua Takadini kiasi hakutamani hali hiyo iwepo, hali hiyo kwa watu wengine ni salama. Kwa hiyo, Takadini amefungwa kwa sababu kwa dhati ya nafsi yake angekuwa na uwezo wa kuzuia jua lisiwake angefanya hivyo lakini anashindwa kwa sababu hali hiyo ni hali ya kijaala.

Kwa namna nyingine, ufungwa wa kijiografia unajitokeza pale mwanadamu anapojikuta amezaliwa kwenye familia au koo au taifa fulani hata kama hakupenda kuwa kwenye koo hizo. Hali hii inajitokeza hata kwenye baadhi ya semi za kiafrika, kwa mfano, semi kama *heri ya kuzaliwa paka Ulaya kuliko kuzaliwa binadamu Tanzania.* Licha ya misemo hiyo, pia ufungwa huu unajidhihirisha kupitia maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu katika kitabu kitukufu cha Quran, anasema:

> *Enyi wanaadaamu, hakika sisi tumekuumbeni kutokana na mwanaume mmoja (Adam) na mwanamke mmoja (Hawa) na kisha tukakufanyieni mataifa na makabila mbalimbali ili mpate kujuana, hakika aliyembora kwenu nyote mbele ya Allah ni mchamungu tu. Hakika Allah ni mjuzi mwenye khabari* (Alhujuraat:13).

Aya hii imedhihirisha ufungwa wa kisaikolojia wa kijiografia na namna unavyomkabili mwanadamu. Mwanadamu hana uwezo wa kujipangia kuwa ni wa kabila au wa taifa fulani bali hupangwa na Mwenyezi Mungu. Aina hii ya ufungwa inajitokeza katika riwaya ya *Takadini*. Mwandishi anamchora mhusika Sekai na mtoto wake namna wanavyochukia kuwa katika ardhi ya mtemi Zvedi. Sekai anachukia kuwa mkazi wa hapo kwa sababu amekuwa akilaaniwa na jamii kwa sababu ya kuzaa *sope*. Kwa sababu hiyo, anahama na kuhamia katika ardhi nyingine ya mfalme Masasa. Mwandishi anasema,

"Mama huyu aliyekuwa akitoroka hakujua alikoelekea. Hata hivyo alikuwa na uhakika kuwa aliachana na watu wa jamii ya mumewe na pia vijiji jirani" (Uk. 21).

Uamuzi huu wa Sekai wa kuhama katika ardhi ya mumewe inadhihirisha kuwa Sekai alikuwa na ufungwa wa kisaikolojia wa kijiografia. Ijapokuwa aliweza kujitafutia uhuru wake kwa kuhama ili awe huru kumlea mtoto wake Takadini ambaye ni *sope.*

## 4.0 Hitimisho na Mapendekezo

Kwa jumla, ufungwa wa kisaikolojia una athari kubwa kwenye jamii na hupelekea mauaji, wizi, kwenda jela, uchawi na ushirikina. Zaidi pia, kila mwanadamu ni mfungwa kijaala kwa sababu mambo mengi yanayomzunguka mwanadamu yametokana na Mwenyezi Mungu. Hivyo, hakuna ambaye yuko huru kwa asilimia mia moja. Ili kuepukana au kupunguza vifungo hivi, mapendekezo yafuatayo yanatolewa kwa serikali, jamii na wanataaluma. Serikali iboreshe huduma za kisaikolojia ili watu washauriwe kuhusu masuala mbalimbali ya kisaikolojia na namna ambavyo wanaweza kukabiliana nayo. Hii itasaidia kupunguza matukio maovu katika jamii, ambayo yanatokana na matakwa binafsi ya kimatamanio yanayoshindwa kutimizwa. Kwa jamii, wito unatolewa kwa wanajamii kukubaliana na hali ya ufungwa wa kijaala, ambao ni vigumu kuuepuka ili kujipunguzia shida za kisaikolojia, ambazo zitapelekea kujikuta kuingia katika mambo maovu katika kuusaka uhuru binafsi. Mwisho, wanataaluma wafanye tafiti zaidi kuhusu dhana ya ufungwa kwa kujikita katika tanzu zingine za fasihi, kama vile ushairi, tamthiliya, semi, na kadhalika. Na zaidi kumakinikia, ufungwa wa kisaikolojia usio wa kijaala umedokezwa katika makala haya.

**Marejeleo**

Badru, Z. (2019). Mfumo dume - chanzo cha ufungwa wa mwanamume: Uhakiki wa semi kutoka jamii za kiafrika. *Journal of University of Namibia Language Centre*, *4*(1), 60–69 (ISSN 2026 - 8297). http://journals.unam.edu.na/index.php/JULACE/article/view/1466

Bakari, S.Y. (2018). *Usawiri wa ufungwa katika methali za Kibondei*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Baraza la Kiswahili la Taifa [BAKITA], (2017). Kamusi kuu ya Kiswahili, Kenya: Longhon Publishers.

Bwaya, M. (2014), Maana ya saikolojia na nafasi yake katika jamii -1

http://bwaya.blogspot.com/2014/08/maana-ya-saikolojia-na-nafasi-yake.html

Duwe, M. (2021). Hatima ya maisha ya waafrika katika bunilizi za Kiswahili: Mwegamo wa kifalsafa. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS)*, *7*(1), 181–190.

Farsy, A. S. (1993). *Quran takatifu*. Nairobi: Islamic Foundation.

Hamad, M. A. (2017). *Suala la ufungwa katika ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka diwani ya sauti ya dhiki na chembe cha moyo*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Hanson, B. J. (2003). *Takadini*. Dar es Salaam: Mathews Book Store & Stationary.

Kijogoo, S. (2021). *Ijue saikolojia*. Dar es Salaam: King Kijogoo Publishers.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mauki, C. (2020). *Msongo wa mawazo: Uelewe na umudu.* Dar es Salaam: Kiwonyi Printes & Media Service.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili [TUKI], (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Nairobi: Oxford Un. Press.

Ponera, S. A. (2019). *Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa nadharia ya fasihi linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Said, Z. (2016).*Usawiri wa ufungwa katika riwaya za Kiswahili: Mifano kutoka katika riwaya ya umleavyo na haini*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Said, Z., & Taib, A.H. (2019). *Fasihi ya ufungwa*. Dar es Salaam: Heko Publisher.

Sengo, N. T. (n.d). *Mke ni waziri mkuu nyumbani mwake*.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake.* Nairobi: Open University Press.